

HALMASHAURI YA MANISPAA KIGAMBONI

Simu: +255 22-2928468
Fax: +255 22-2928469
Barua pepe:
info@kigamboni.go.tz
Tovuti: www.kigamboni.go.tz



S.L.P. 36009,
KIGAMBONI,
DAR ES SALAAM,
TANZANIA.
Tarehe; 16/9/2019

TANGAZO LA ZABUNI

WITO WA FUNDI KWA AJILI YA UJENZI WA MWALO WA SAMAKI WA BUYUNI- KATA YA PEMBA MNAZI.

1. Mkurugenzi wa Halmashuri ya Manispaa ya Kigamboni anapenda kuwaalika Mafundi wa Ujenzi katika Manispaa ya Kigamboni kutuma maombi ya Fundi Mkazi (**Local Fundi**) Kwa ajili ya ujenzi wa Mwalo wa Samaki wa Buyuni katika Kata ya Pemba Mnazi.
2. Maombi yawe katika nakala halisi na nakala nyingine moja ifungwe vizuri katika bahasha iliyowekwa LAKIRI (**Seal**) na Maombi yaandikwe kwa:-
**Katibu wa Bodi ya Zabuni,
Halmashuri ya Manispaa Kigamboni
S.L.P 36009
Dar es Salaam.**
3. Maelezo ya kazi hii yanapatikana katika Vionjo (**Specifications**) ambayo nakala zipo katika Ofisi ya Manunuzi Jengo la Mkurugenzi Manispaa ya Kigamboni
4. Wanaotakiwa kuomba ni Mafundi Binafsi "**Local Fundi**" na **SIYO** Kampuni.
5. Muombaji anapoomba anapaswa kutamka, kuzingatia na kuambatanisha vitu vifuatavyo:-
 - a. Muombaji awe mtu mzima (kuanzia miaka 18) na mwenye akili timamu.
 - b. Muombaji aambatanishe nakala ya cheti/vyeti vinavyoonyesha amefuzu Elimu ya Ufundi Ujenzi.
 - c. Muombaji aonyeshe eneo anapoishi (Wilaya, Kata na Mtaa) na namba ya simu ya Mkononi.
 - d. Muombaji asiwe anadaiwa **AU** kuwa na Mgogoro na Halmashuri ya Manispaa ya Kigamboni.

- e. Muombaji anapaswa kufanya utafiti wa kutosha kabla ya kuomba zabuni ikiwa ni pamoja na kutembelea eneo la kazi (**site visit**) kusoma na kuelewa michoro ya kazi husika.
- f. Muombaji asiwe Mtumishi, Diwani wa Halmashauri ya Manispaa ya Kigamboni **Au** mtu yeyote mwenye **MGONGANO** wa Kimaslahi katika kazi hii.
- g. Kwa kutokuelewa Kipengele chochote unaombwa kufika Ofisi ya Manunuzi iliyopo Halmashuri ya Manispaa ya Kigamboni kwa ajili ya kupatiwa Ufafanuzi zaidi.
- h. Muombaji anatakiwa kutaja maeneo aliyowahi kufanya kazi zinazofanana na kazi hii.
- i. Mwisho wa Kupokea maombi haya ni tarehe **19/09/2019** siku ya Ijumaa Saa **4.00** Asubuhi na ufunguzi utafanyika Hadharani katika **Ofisi ya Manunuzi Halmashauri ya Manispaa Kigamboni Saa 4.30** asubuhi.
- j. Maombi yatakayochelewa kurudishwa baada ya saa **4.00** asubuhi hayatapokelewa.

**Mkurugenzi wa Manispaa.
Halmashuri ya Manispaa ya Kigamboni**